

Mustapha na EL-HANOUCHI

Katika kijiji kimoja kandokando mwa milima aliishi mtu aliyeitwa Mustapha. Alikuwa yatima na mpweke, kwa sababu baba yake na ndugu zake wengine waliuwawa kikatili na khabila majirani zao. Alijua wazi kwamba atakapokuwa mtu mzima kiasi cha kuota ndevu, wale waliowauwa ndugu zake wangemtafuta ili naye wamuue. Lakini hakuogopa. Akasema: "nitatumia maarifa na akili zangu ili kujilinda."

Mustapha alipoendelea kukua na kuwa mtu mzima, siku moja akitokea katika kazi yake mashambani alikutana na mtu mmoja mgeni aliyeavaa vizuri sana. Mtu huyu aliongea naye kwa upole huku akitaka kujua habari zake. Mustapha aliridhia uhusiano huu wa kirafiki, kwa sababu ni mara chache sana wageni wanafika kijijini kwake. Siku chache baadaye alikutana na mtu yule yule nje kidogo ya kijiji na akasalimiana naye kwa furaha kubwa. Yule mgeni akasema: "Ninaishi mbali sana kutoka hapa: Nilimjua baba yako na familia yake na niliwasaidia sana. Sasa naona kuwa wewe umekuwa mtu mzima; kijana mtanashati na mwenye akili. Nimeona niente ili nione kama nitaweza kuwa wa msaada kwako kama nilivyokuwa kwa baba yako, kwa sababu kwa hakika unapoteza muda wako mwingi kijijini mahali ambapo hakuna kitu chochote zaidi ya mashamba, na hakuna njia ya kipato ila miiba na mizeituni"

Mustapha aliguzwa na maneno ya yule mgeni na alipomwalika katika mkahawa fulani kwa chakula alikubali. Siku ile ilikuwa siku nzuri sana, jua likizama na kijiji kilijaa watu waliokuwa wakitembea huku na kule. Mle katika mkahawa kulikuwa na mzee mmoja wa pale kijijini, alikaa pembeni akimwangalia yule mgeni na Mustapha wakiongea kwa furaha huku wakiendelea kula. Baadaye yule mgeni akalipa ile gharama ya chakula. Mustapha akamshukuru yule mgeni naye akaondoka.

Mustapha alisimama pale mlangoni, akifikiria jinsi alivyokuwa na bahati kwa kikutana na. mtu mkarimu kiasi kile, aliyekuwa tayari kumtoa katika hali ile duni. Aliona nyakati za furaha zikinyemelea.

Baada ya yule mgeni kuondoka, yule mzee wa kijji aliyeitwa Si Bualam, alimsogelea Mustapha na kumwambia; "Njoo, nifuate kijana wangu. Nina jambo nataka nikwambie". Huku akitafuta njia yoyote ya kutokuwa kazini, Mustapha akakubali. Wakatafuta mahali pazuri pa kukaa chini ya miti, nje kidogo ya kijiji.

Si Bualam, akazungumza kwa makini sana na kumwonya yule kijana: "Kijana wangu, jihadhari na mgeni anayetafuta urafiki na wewe. Yeye ni wa kabila la El-Hanouchi na amekuja na mawazo maovu. Usihadaike na kujionyesha kwake kwako kama rafiki. Kwa sababu sasa amekuju, hatapumzika mpaka akuue. Hana ujasiri wa kukushambulia hadharani, kwa hiyo anajaribu kukulaghai ili uende naye katika sehemu fulani iliyojificha ambapo atakuua".

Maneno hayo ya huyu mzee yalimsumbuwa sana Mustapha. Ukweli ni kwamba alikuwa tayari ameingia katika mtego wa yule mgeni ambao ulikuwa umemweka katika kufikiria juu ya furaha ya maisha yake ya baadaye. Si Bualam alisema kwa kirefu kiasi ambacho mawazo ya Mustapha yakaanza kupotea na kugundua kwamba alikuwa hatarini. Mwisho akasema: "Asante sana, Si Bualam kwa kunionya. Nitakuwa mwangalifu sana wakati mwingine akija".

Si Bualam alizungumza kwa utaratibu: "Kijana wangu, kwa nguvu zako na kwa hekima yako mwenyewe hutaweza kijiokoa. El-Hanouchi ni mwenye nguvu na mkaidi. Atakulaghai mpaka umfuate kama kondoo kwa mchinjaji. Kuna mahali pa uhakika pa usalama ambapo nitakuambia. Unaiona ile milima kule upande wa mashariki? Katika milima ile kuna mji mzuri sana wa El-Melija. Mwana wa Mfalme wa El Melija alikuwa rafiki wa baba yako. katika maisha yake yote. Siku moja aliingilia kati wakati wa mauaji ya baba yako na kwa sababu hiyo akawa adui wa kabilia la El-Hanouchi. Walijaribu sana kumuua Mwana wa Mfalme. Matokeo yake wale wa El-Hanouchi walifukuzwa katoka mji wa El-Melija; hawawezi kuingia huko, la sivyo watauawa. Ikiwa utaweza kutorokea katika mji huo, adui hataweza kuguza unywele wa kichwa chako. Chukua ushauri wangu na utoroke kabla adui yako hajaja. sasa nenda kwa amani!"

Siku zilizofuata Mustapha alisumbuka sana nafsini mwake. Wanakijiji walisema kwamba walimwona El-Hanouchi pale kijijini. Lakini Mustapha alikipenda sana kijiji chake na hivyo hakutaka kukiacha. Akakawia kuondoka kwenda katika sehemu ile asiyoijua. Siku zikapita na majuma mengi pia yakapita . Siku moja alipokwenda katika mkahawa pale kijijini, alimkuta El Hanouchi ameketi karibu na mlango. Alimsalimia Mustapha na akamwambia alikuwa na jambo alilotaka kumwambia kwa siri. Mustapha akachanganyikiwa, kati ya ushauri aliopewa na Si Bualam na yule mgeni. Mwisho hamu ya kutaka kusikia kutoka kwa yule mgeni ikamfanya afuatane na El Hanouchi.

"Najua kwamba wapumbavu wengi katika kijiji chako wamekuonya dhidi yangu," El- Hanouchi alisema, "lakini nitakuthibitishia wazi kwamba nia yangu ni njema. Wewe ni kijana mwenye nguvu ambaye unaweza kunisaidia. Nitahakikisha unafaidika kwa muda wako utakaoutumia kwa ajili yangu. Kandokando ya msitu nimegundua mahali ambapo wezi wanaficha mali tangu zamani. Ukinisaidia kumalizia kuchimbua mali hiyo nusu itakuwa yako."

Ahadi hii ilikuwa jaribio kubwa sana kwa Mustapha. Alivutiwa na kuwa na matumaini makubwa ya utajiri. Wakakubaliana waende mahali pale mara mwezi utakapotoka kama saa nane usiku. Mustapha akaamua kulala katika choo cha umma ili asije akagundulika wakati atakapoondoka.

Wakakutana kandokando ya msitu na kwa mwangaza wa mbalamwezi wakaweza kuona mahali pa kuingilia katika ficho la wezi. Mustapha aliingia wa kwanza katika msitu akifuatiwa na El-Hanouchi. Mustapha akaanza kunyong'onyea kwa sababu hakukuwa na dalili zozote za hazina - wala dalili ya kuchimbwa au vifaa vya kuchimbria ama uchafu. Mara yakamjia mawazo jinsi ilivyokuwa rahisi kwa El-Hanouchi kumuua. Hapakuwa na mtu karibu na watu, wote walikuwa wamelala. Alipomwangalia El-Hanouchi aliona kitu kiovu machoni mwake na moyo wake ukaanza kudunda kwa hofu kubwa.

Mara ikasikika sauti ya Si Bualam barabarani akiimba, angalau sauti ya mtu aliyemjua.. Kabla El-Hanouchi hajawenza kumzuia Mustapha aliruka akatoka na kumkimbia rafiki yake. "Mungu apewe sifa" Si Bualam akasema. "Njoo haraka, nifuatel!" baada ya kutulia, Mustapha akamuuliza Si Bualam: "Rafiki yangu, ilikuwaje ukaweza kunifuata usiku huu?" Si Bualam akajibu: "Mimi pia nililala katika nyumba ya bafu. Nilijua kwamba El-Hanouchi alikutembelea jana na nilikuwa nikiangalia nione ni nini kitatokea. Ulipoamka na kuondoka nilikuifuata. Na

sasa kijana wangu amini maneno yangu. Jambo ovu limepangwa kwa ajili yako. El- Hanouchi ana kiu na damu yako na haitaisha mpaka akuue. Kimbilia El-Melija kijana wangu. Usipoteze wakati, tena hata kwa kuiaga nyumba yako". Onyo la Si Bualam lilikuwa la haraka sana na Mustapha alishikwa na woga kiasi cha kuondoka kuelekea El-Melija mara moja.

Alasiri ya siku iliyofuata aliona kwa mbali kuta za mji ziking'aa. Moyo wake ukajawa na mashaka. Je, Mwana wa Mfalme atamkaribisha mjini El-Melija? Na El-Hanouchi Je? Kweli alikusudia kumwua Mustapha? Kama ndivyo, bila shaka anaweza kuwa anasubiri nje ya milango ya El-Melija!

Asubuhi kulipopambazuka, Mustapha akakaribia milango ya El-Melija. Milango ilifunguka wakati wa pambazuko. Jua liliyopambazuka kwa utukufu. Aliona kwa mbali milango ikiwa imefunguliwa kwa ajili ya kumlaki. Alipokuwa akitokezea akaona kwa mbali mtu kama adui yake. Mustapha alikimbia kama upepo na El Hanouchi akimfuata nyuma yake. Katika milango ya mji Mwana wa Mfalme akiwa katikakati mwa wazee, walikuwa wamekusanyika kumkaribisha.

Alipokaribia lango, hatua chache tu ndizo zilimtenga Mustapha na adui wake mkuu El-Hanouchi. El Hanouchi alilenga kisu chake juu ya kichwa cha kijana. Huku akiwa amechoka sana, Mustapha alijirusha katika lango na kuingia mjini. Mwishowe alikuwa salama! Mwana wa Mfalme alimwinua na kumwingiza na kumweka mahali salama mjini. El-Hanouchi alijua hangeweza kumfuata kijana huyo zaidi ya hapo. Alimwangalia kijana kwa hasira pamoja na Mwana wa Mfalme kisha akaondoka.

Mwana wa Mfalme akazungumza na mzee mmoja. "Namjua kijana huyu. Ni mtoto wa rafiki yangu aliyeuawa na watu wa kabile la El-Hanouchi. Furahini pamoja nami kwa sababu yuko salama hapa kwetu." Mustapha akajisikia kuwa na furaha kubwa na amani ikiwa juu yake. - Alikuwa ameepuka mgeni mbaya aliyejaribu kumlaghai na kumwingiza katika mauti. Atakaa hapa kwa amani, mahali ambapo adui hawezi tena kuthubutu kumkabili Mwana wa Mfalme anayetawala.

Mpendwa msomaji, kumekuwa na uadui mkubwa kati ya binadamu na dhambi tangu wakati wa baba yetu Adamu mpaka sasa.

Kuna sehemu moja tu unaweza kukimbilia kuepuvana na dhambi, mahali palipochaguliwa na Mungu. Napo ni kwa Yesu Masihi, ambaye alithibitisha kwa maisha yake na kwa ufufuko wake kutoka kwa wafu na kwamba ana nguvu za ki-Mungu za ushindi dhidi ya dhambi. Kama Biblia takatifu inavyosema: "mshahara wa dhambi ni mauti,' bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu" (Warumi 6:23). Yesu pekee ndiye anayeweza kusema; "Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake" (Yohana 1:12).

Masihi amefungua mlango kwa ajili yetu kuingia katika sehemu salama. Anasema: "Mimi ni

mlango; mtu akiingia kwa mimi, ataokoka; ataingia na ataokoka, naye atapata malisho" (Yohana 10:9). Yesu anasema pia kwa wote wanaomjia: "*Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu*" (Yohana 10:28).

Unaweza kuja kwa Yesu Masihi hivi sasa kwa maisha mapya. Amesimama katika lango la "Mji wa Uzima" tayari kukukaribisha na kukukinga dhidi ya nguvu za dhambi. Unachohitaji kufanya ni kufungua moyo wako kwa Yesu Masihi. Sikiliza mwaliko wake:

Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenyewe kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigio wangu ni mwepesi. "(Math. 11:28-30)

Rafiki mpendwa, unaweza kujigundulia mwenyewe kwa nini Yesu Masihi pekee ndiye anaweza kukusamehe dhambi zako na kwa nini yeye ndiye kimbilio la salama katika maisha haya na katika hukumu inayokuja.

Ikiwa unapenda kujifunza zaidi juu ya Yesu Masihi, tuko tayari kukutumia vijitabu vyatukusaidia zaidi:

‘Jitahidi Kulinganisha’
Kuwa mwumini kwa hiari

Tafadhali andika jina lako na anwani ya barua pepe vema, kisha utume kwa:

info@lifechallenge.de

Tukutane tena kwa masimulizi mengine